## WATOTO WADOGO KATIKA MAZINGIRA YA BIASHARA

- Japo ni asilimia ndogo ya wanawake wanakwenda na watoto wao sokoni, EfG ilifanya utafiti mdogo kwa kuwahoji wanawake sita (6) ili kujua ni kwa nini wanakwenda na watoto wao katika biashara zao. Wanawake hawa walitaja sababu zifuatazo: Ni mzazi pekee aliyebaki (mjane), anatumia muda mwingi kuhudumia familia yake ili iweze kupata mahitaji muhimu ya maisha yao, mfano chakula, malazi na mavazi.
- Umasikini pia ni chanzo kinachowafanya wanawake kwenda na watoto kwenye sehemu za kufanyia biashara kwa sababu hawana uwezo wa kumlipa mfanyakazi wa ndani.

Mazingira ya soko yameonyesha kuwa si salama kwa watoto wadogo kutokana na uchafu, harufu kari, pamoja na vumbi ambalo linaweza kusababisha madhara ya kiafay kwa watoto hao kama magonjwa ya mlipuko, kifua na ngozi.

Maria I. *ana umri wa zaidi ya miaka 30, na anafanya biashara zake katika soko la Tabata muslimu takribani mwaka mmoja sasa,anauza vitunguu,papai na mboga mboga.kila siku saa 11 alfajiri anakwenda soko la Tandika kutafuta bidhaa na mtoto wake mwenye umri wa mwezi mmoja kwa ajiri ya kuuza katika soko lake la Tabata muslimu.anasema…"siwezi kwenda na watoto wangu wote badala yake na mchukua mtoto wangu wa mwezi mmoja na huyu wa miaka mitatu nakwenda nao kibaruani (yaani sokoni)baaba ya kutoka Tandika… lakini sina budi kwenda na watoto wangu sokoni sababu baba yao amefariki mwaka huu na mimi ndio ninajukumu la kulea familia…isitoshe sina mtaji wa kuniwezesha kupanua biashara yangu na kumpeleka mwanangu chekechea maana ana umri wa kwenda shule".*

## UKATILI WA KIJINSIA MASOKONI

Ukatili wa kijinsia unaongoza katika masoko ni udhalilishwaji wa maneno unaofanyika kwa asilimia 37 na bughudha za kijinsia za makusudi ni asilimia 39.7. Lugha chafu (matusi) pamoja na wanaume kutowalipa fedha hasa baada ya kupata huduma ya mama lishe. Ni asilimia 31.6 tu wanawake waliopitia ukatili waliamua kuripoti kwa vyombo husika kama viongozi wa soko au katika vyombo vya sheria.




## HAKI YA KUTOA NA KUPOKEA TAARIFA NA ELIMU

Ni asilimia ndogo sana ya wanawake wa masokoni wanaelewa wa kutosha juu ya masuala muhimu ya maisha na biashara zao. Mfano ni asilimia 10.3 waliainisha haki ya kumiliki biashara, asilimia 8.6 haki ya kumiliki mali, na asilimia 6.9 haki ya kusikilizwa pamoja na asilimia 6.3 haki ya kukopa kwa riba nafuu. Uelewa juu ya haki za kisheria na haki za binadamu na taarifa muhimu zinazohusu biashara zao ni mdogo. Japo, asilimia 50 ya wanawake wanapata ushauri wa kisheria pindi wanapohitaji, ni asilimia 16.7 tu ndio wanaofahamu taasisi au mashirika yanayotoa ushauri wa kisheria. Utafiti uligundua wanawake walio wengi hupata ushauri wa kisheria toka kwa watu binafsi.

## FURSA ZA WANAWAKE.

- Kufanya maamuzi

  Takribani asilimia 62.1 ya wanawake wamesema wanafanya maamuzi ya mipango na maendeleo ya familia zao
- Uhuru wa kumiliki mali

  Inatia hamasa kuona takribani asilimia 90.1 ya wanawake wafanyabiashara wanaona wana haki kumiliki mali katika familia.
- Majukumu ya nyumbani

  Asilimia 24.5 ya wanawake wanaona mwenye jukumu la kwanza katika kuhudumia familia ni mwanamke, japo asilimia 46.4 wamesema kila mwanafamilia ana jukumu la kuhudumia familia wakati asilimia 28 wamesema mwanaume ndio mwenye jukumu la kwanza la kuhudumia familia.
- Mafunzo

  Wanawake walio wengi wapo tayari katika kufanya mafunzo mbalimbali ambayo yataweza kuwasaidia katika kuinua biashara zao na kuondokana na umasikini. Asilimia 39.1 wapo tayari kufanya mafunzo siku ya mapumziko na asilimia 36.8 wanaweza kufanya mafunzo jioni.

## CHANGAMOTO

- Kutokuwepo kwa mifumo rasmi inatoa nafasi na fursa kwa wanawake waliokatika sekta isiyo rasmi kushiriki katika michakato na maamuzi yanayohusu maisha yao katika ngazi zote ikiwemo wilaya na taifa.
- Kuwepo kwa wadau wachache wanaolenga makundi ndani ya sekta iliyo rasmi ili kuweza kukabiliana na changamoto za kundi husika.
- Ni asilimia 31.6 ya wanawake wamesema vikundi vyao katika masoko havipo katika kutetea maslahi yao kama wafanyabiashara. Masoko mengi hayana vikundi vya wanawake na hata kama vikiwepo vipo tu kwa ajili ya kushiriki katika kamati za soko na si kuwasaidia wanawake wa soko husika katika kutatua kero zao zinazo wakwamisha katika kuinua biashara zao.
- Nusu ya wanawake hawapati huduma za kisheria. Ni ngumu kwao kugharamia upatikanaji wake au taasisi zinazotoa huduma hizo ni chache.

Equality for Growth (EfG)

# WANAWAKE SOKONI

EQUALITY FOR GROWTH (EfG) ni shirika lisilo la kiserikali lenye lengo la kuinua nafasi ya wanawake katika nyanja mbalimbali ikiwemo ya kiuchumi. Wanawake walioajiriwa au kujiajiri katika sekta isiyo rasmi ni walengwa wakuu na wadau wa shirika hili.EfG inajenga uwezo wa wanawake hawa kutambua fursa juu ya masuala yanayohusu maisha yao. Ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa kwa kundi hili EfG inaamini ushirikishwaji na ushiriki wa wanawake na wanaume kwa pamoja utapelekea kuwepo kwa maendeleo endelevu.

## DIRA

Dira of EfG ni kuona hakuna vikwazo vyovyote vya kijinsia kwa wanawake walio katika sekta isiyo rasmi na wanawake wakiwa mbali na aina zote ya unyonyaji.

## DHIMA

Dhima ya EfG ni kuinua maendeleo ya sekta isiyo rasmi Tanzania, hususani wanawake kwa kupunguza umaskini kwa njia ya kutoa mafunzo ya haki za binadamu na msaada wa kisheria, kuwezesha kuwepo kwa fursa sawa za kibiashara kwa wanawake, pamoja na kushawishi utungaji wa sera zinazoinua wanawake na kujenga uwezo kwa wanawake na wanaume.

## MALENGO YA EfG

Malengo makuu ya EfG ni kusaidia jamii ili kuona wanawake na wanaume wana haki na nafasi sawa ya kumiliki mali na shughuli za kiuchumi, utawala na kuinua maendeleo ya sera za uchumi na kijamii. EfG imeanzishwa kwa lengo la kusaidia wanainchi waishio mijini na vijijini

EfG imeweka malengo yafuatayo:

- Kuhamasisha na kusaidia wanawake walio katika nyanja ya kuichumi kujenga umoja na kujenga uwakilishi wao kwa lengo la kuwapa uwezo wanawake wajasiria mali kutambua haki zao.
- Kuwezesha mazingira ya kutambulika kwa haki za wanawake wafanyakazi na wazalishaji.
- Kutoa huduma mbalimbali zikiwemo za ushauri wa kibiashara, msaada wa kisheria, mazingira ya upatikanaji wa taarifa muhimu, sahihi na kwa wakati katika maswala ya yanayohusu biashara zao, sheria, mikataba, ardhi, kodi na maswala yote yanayohusu biashara.
- Kusaidia wanawake na wanaume wote kwa sawa kumiliki, kutawala, kutumia ardhi na vyanzo vingine vya uzalishaji ili kuinua maisha yao.
- Kufanya utafiti katika sera, sheria na biashara/masoko kwa wanawake walio katika sekta isiyo rasmi na kuondoa (reform) sera zinazokandamiza usawa wa kijinsia.
- Kushirikiana na taasisi na mashirika mengine ndani na nje ya nchini ambayo yana malengo yanayoshabihiana na EfG.

## MRADI WA WANAWAKE MASOKONI

Mradi wa wanawake masokoni umeanza rasmi Oktoba, 2011 katika masoko 18 yaliyopo katika Manispaa ya Ilala, jijini Dar-es-Salaam kuwawezesha wanawake kuboresha biashara zao na mazingira ya kuendesha biashara hizo. Mradi unalenga kuinua sauti na umoja wa wanawake masokoni, kujenga uwezo wao katika kusimamia biashara, kuwezesha kuwepo kwa upatikanaji wa huduma muhimu kwa wanawake na kuwawezesha kuwa washiriki muhimu katika kuendeleza masoko yao kwa kushirikiana na uongozi wa masoko na Manispaa husika. Mradi huu ni zao la utafiti ulioendeshwa na EfG mwaka 2009

## UTAFITI

Kutokana na utafiti uliofanywa na EfG mwaka 2009 katika masoko kumi (10) yaliyoko katika Manispaa ya Ilala, Dar-es-Salaam yafuatayo yalionekana:

## AINA NA MAZINGIRA YA BIASHARA

### Aina ya biashara

Wanawake wengi katika masoko wanaendesha biashara ya mama lishe(36.5%). Wengine hujishughulisha na uuzaji wa nguo na mitumba (13.2%), mboga mboga (6.3%), viungo (5.2%), na samaki (5.2%).




### Umiliki wa biashara

Ni asilimia 67.2 ya wanawake masokoni ndio wanaomiliki biashara wanazoendesha.

### Umiliki wa eneo la kufanyia biashara

Wanawake walio wengi si wamiliki rasmi wa maeneo ya kufanyia biashara. Asilimia 67.2 ya wanawake wafanyabiashara hawamiliki maeneo ya kufanyia biashara zao.

### Vifaa vya biashara

Asilimia 74.7 ya wanawake wanamiliki vifaa vya kufanyia biashara zao, lakini vifaa hivyo ni vya zamani na visivyo na ubora. Asilimia 72.9 ya wanawake hawamiliki vifaa vyote vya biashara, vingi hukodishwa au kuazimwa.

### Mtaji wa kuanzia biashara

Wanawake walio wengi masokoni wanaanza kufanya biashara kwa mtaji usiozidi Tz.100,000/- ni asilimia 37.4.




### Chanzo cha mtaji wa kuanzia biashara

Kuna maswali mengi ya kujiuliza ni asilimia ngapi ya wanawake wanapata mikopo yenye riba nafuu ili kuendeleza biashara zao. Ni asilimia 44.3 ya wanawake wanajitafutia mitaji kupitia vikundi vyao wenyewe vya kuweka na kukopa, mfano 'UPATU'.
Asilimia 81.6 ya wanawake masokoni hawajawahi kupata mkopo kupitia benki wakati asilimia 66.1 hawana akaunti ya benki. Ni asilimia 5.7 ya wanawake ndio wamewahi kupata mkopo kupitia vikundi vya kuweka na kukopa. Sababu zinazowazuia wanawake kufikia mikopo katika taasis za fedha na mabenki ni pamoja na kutotimiza masharti ya mkopo kama kukosa dhamana na hofu ya kukopa.

## UENDESHAJI WA BIASHARA

- Mauzo kwa siku
  Utafiti umeonyesha kuwa asilimia 62.1 ya wanawake wengi wanauza chini ya Tz.30,000/- kwa siku na asilimia 60.9 hupata faida chini ya Tz.7,000/- kwa siku.
- Muda wa kufanya biashara.
  Asilimia 59.2 ya wanawake wanafanya biashara kuanzia masaa 6 hadi 10 kila sikukuanzia jumatatu mpaka ijumaa.

Amina H: *Nafanya biashara takribani miaka 3 sasa, biashara ya kuuza nyanya. Kila siku huamka saa 10 alfajiri, husafisha nyumba na kuandaa chai. Ikifika saa 11 alfajiri naanza safari ya kutembea kwa mguu kuelekea sokoni,mwendo wa saa 1. Kutokana na kutumia muda mwingi kutembea hufika kwenye biashara yak e nikiwa nimechelewa na na kukuta wenzangu wameshauza. Amina anafikiria kubadilisha biashara lakini hana mtaji wa kufanya biashara nyingine.*

- Mtaji ni kikwazo cha kukua kwa biashara kwa wanawake wengi Kuna matatizo mengi yanayokwamisha kufanikiwa kwa biashara kwa wanawake wengi. Kukosekana na mtaji wa kutosha kulionekana kuwa ni tatizo kwa zaidi ya robo ya wanawake walio sokoni (asilimia 27).

## HAKI YA KUFANYA MAAMUZI NA KUSHIRIKI KATIKA UONGOZI

Ni wanawake asilimia 19 walioshika nafasi za uongozi ukilinganisha na asilimia 81 ya wanaume. Mbali na changamoto zilizoonekana za kutokuwepo na mikakati thabiti katika masoko na Manispaa kujenga fursa za wanawake kuwa viongozi pia wanawake wameonyesha kutokuwa na hamasa ya kugombea nafasi za uongozi. Ushiriki wa wanawake katika maamuzi kwa ujumla haujawa bayana na wenye mafanikio.